**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HOTUBA YA KATIBU MKUU WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI – UCHUKUZI KATIKA KIKAO CHA KWANZA CHA BARAZA LA LATRA CCC**

**Tarehe:** 19 APRIL 2021

**Mahala:** Ukumbi wa Mikutano Ghorofa ya 27 Jengo –TPA Dar es Salaam

---

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kwa kutujalia neema ya kukutana hapa kwa ajili ya kusimamia shughuli hii muhimu ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC). Pili ninawapongezeni ninyi wote, kwa kuteuliwa na Mh. Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa Awamu hii mpya ya Sheria Mpya ya LATRA kwa nafasi ya Wajumbe wa Baraza. Hongereni sana.

Nawashukuru wote pia kwa kukubali uteuzi huo na kuhudhuria kikao hiki muhimu cha leo kwa ajili ya kuchagua Mwenyekiti wa kusimamia shughuli za utendaji kazi za Baraza. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito ya kiofisi au binafsi lakini kwa kutambua umuhimu wa uchaguzi huu na kwa kuanza kutekeleza

majukumu ya Baraza, mmeacha shughuli zenu ili kwa pamoja tuweze kushirikiana.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza LATRA CCC ni kwa mujibu wa Kifungu Namba 29 (2) cha Sheria namba 3 ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, (LATRA) ya Mwaka 2019. Sheria hii, katika kifungu cha 29(7) inaelekeza zaidi kuwa, baada ya Wajumbe kuteuliwa, watakaa kwa pamoja na kuchagua miongoni mwao Mwenyekiti wa Kuongoza Baraza kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu (03) kuanzia tarehe ya uteuzi wa Wajumbe.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Sheria inaelekeza Kuwa, jumla ya Wajumbe wa Baraza ni Saba (07) tofauti na ilivyokuwa hapo awali wakati wa Sheria ya SUMATRA ambapo wajumbe wangeweza kuwa hadi kumi (10). Ila kutokana na Mabadiliko ya Sheria sasa, tuna wajumbe watano (05) watakao hudumu kwa kipindi cha miaka mitatu (03) na Wajumbe wengine wawili (02) watakao hudumu kwa kipindi cha miaka minne. Hivi Sasa Mh. Waziri amekamilisha uteuzi wenu wa Wajumbe Watano, ambapo mnatakiwa kuanza kazi mara moja wakati utaratibu wa kuwapata wajumbe wengine wawili (02) unaendelea.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Nataka kuwajulisha Majukumu ya Baraza kama ilivyo katika sharia kuwa ni:

(i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri kwa njia ya Reli, usafiri wa umma kwa njia ya barabara, usafiri wa chini ya ardhi na usafiri kwa njia ya waya, kwa kuwasilisha, kupata maoni na tarifa na kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana na wadau wa sekta mbalimbali zinazodhibitiwa;

(ii) Kupokea na kusambaza tarifa na maoni mbalimbali kuhusu masuala yanayowagusa watumiaji wa huduma zinazosimamiwa na LATRA;

(iii) Kuunda kamati za Watumiaji wa huduma za usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na LATRA katika Mikoa na Kushauriana nazo;

(iv) Kushauriana na wadau , Serikali na makundi ya watumiaji kuhusu huduma; na

(v) Kufanya utafiti juu ya maslahi, haki, wajibu na masuala mengine yanayogusa watumiaji.

Aidha, utekelezaji wa Majukumu haya yanapaswa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali, inayotolewa na Serikali mara kwa mara.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Kwenye Ripoti ya CAG ya hivi karibuni, LATRA CCC imetajwa katika taarifa hiyo kuwa Baraza la Ushauri la huduma la LATRA lilikuwa likilipa viwango vikubwa (shilingi 500,000/=) kwa watumishi kama posho ya kujikimu kwa siku. Taarifa hii, sio nzuri kwa Wizara na kwa

Baraza pia. Jukumu lenu la kwanza ninaloagiza ni kuhakikisha viwango vyote vitakavyotumika katika Baraza, vinapitiwa na vifuate utaratibu wa kupata idhini kutoka kwa Msajili wa Hazina.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Kama tulivyosikia taarifa fupi ya hali ya Ofisi ya Baraza kuwa, Miundombinu ya ofisi sio mizuri, kodi kubwa ya pango, vifaa vingi ni chakavu, oneni ni kwa namna gani ya kusaidia, Watendaji wa Baraza kuhamia kwenye majengo ya Serikali na kupata vitendea kazi vipya ili kazi ya kujenga Taifa iweze kufanyika kwa wepesi.

Aidha, ninaliagiza Baraza kuhakikisha linafanya kazi kwa ukaribu na LATRA ambaye ni Mdhibiti ili kutatua changamoto zilizopo katika Sekta. Kwa mfano, kumekuwa na matishio mengi ya mara kwa mara kutoka kwa watoa huduma, hasa kugomea suala la tiketi Mtandao, kugomea kifaa cha kuratibu mwenendo wa mabasi na mambo kadha wa kadha.

Andaeni vipindi vingi vya kuwaelimisha watumiaji wa huduma hizi (Abiria) ili waone umuhimu wa kudai haki zao. Ni Imani yangu kuwa, Mkishirikiana kwa Pamoja, mtatatua changamoto nyingi kwenye Sekta hii.

**Ndg, Wajumbe wa Baraza,**

Kwa kuwa, wajibu wangu kwa siku ya leo, ni kusimamia uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza, ili aweze kutekeleza niliyoagiza, naomba niwakumbushe utaratibu ulioainishwa kwenye kanuni ya Baraza.

1. Baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa baraza watachagua Mwenyekiti wa Baraza kutoka miongoni mwao;
2. Kila Mjumbe aliyeteuliwa ana nafasi sawa ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza;
3. Wajumbe wa Baraza watapendekeza majina mawili (02) miongoni mwao, kwa mtu atakaye shika nafasi ya kuwa Mwenyekiti;
4. Uchaguzi wa Mwenyekiti utafanywa kwa kupiga kura za Siri;
5. Yeyote atakayepata kura nyingi ndie atakayekuwa Mwenyekiti; na
6. Ikiwa kura zimefungana, Msimamizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kuamua ni nani awe Mwenyekiti.

Baada ya kusema hayo, ninawatakieni upigaji kura mwema.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

**KATIBU MKUU - UCHUKUZI**